

HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI (CMT) KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI HADI MACHI, 2022) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 TAREHE 08/04/2022

A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA.

Na.	JINA KAMILI	WADHIFA/CHEO
1.	Ndg. Apolinary Seiya	Kaimu Mkurugenzi - Mwenyekiti
2.	Ndg. Fredrick Kayombo	Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala - Katibu
3.	Ndg. Charles Tuyi	Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
4.	Ndg. Yasin Kiula	Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
5.	Ndg. Esther Kandoga	Afisa Ushirika
6.	Ndg. Annie Kundi	Kaimu Mkuu wa kitengo cha Nyuki
7.	Ndg. Matilda Yasin	Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
8.	Ndg. Erick Anthony	Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
9.	Ndg. Joseph Kisege	Afisa Habari na Mawasiliano
10.	Ndg. Criss. Nyamvugwa	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
11.	Ndg. Filbert Kombe	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi
12.	Ndg. Gutan Mbogo	Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
13.	Ndg. Nassoro H. Mkwanda	Mkuu wa Idara ya Fedha
14.	Ndg. Suma Mwilafu	Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi

A. SEKRETARIETI

NA	JINA KAMILI	WADHIFA
98 1.	Ndg. Rukia Jaka	Mwandishi wa Kikao

MUHT: Na.1/HM/MAF/CMT/MAR/2021/2022- 08/04/2022: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha kawaida cha Kamati ya Watalam ili kujadili taarifa za utekelezaji kwa kipindi cha mwezi Machi, 2022. Aidha, aliwaomba wajumbe kuchangia hoja kwa agenda zitakazowasilishwa.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 07:55 mchana.

MUHT: Na.2/HM/MAF/CMT/Q3/2021/2022- 08/04/2022: KUTHIBITISHA AGENDA

Wajumbe walithibitisha jumla ya agenda Ishirini (20), ili zitumike kuongoza kikao husika. Agenda zilikuwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.

3. Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha robo ya tatu (Januari hadi Machi, 2022).

4. Kufunga kikao.

MUHT: NA.7/HM/MAF/CMT/Q3/2021/2022- 08/04/2022:TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI HADI MACHI, 2022)

Ilielezwa kuwa, kwa mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri ya Mji Mafinga iliidhinishiwa kukusanya, kupokea na kutumia jumla ya kiasi cha Sh. 7,842,388,966.00 ikiwa ni fedha za miradi ya maendeleo kutoka Mapato ya Ndani Sh. 1,747,954,000.00, Serikali Kuu Sh. 2,047,832,826.00 na Wahisani Sh. 4,046,602,140.00. iliendelea kufafanuliwa kuwa kwa kipindi cha robo ya tatu (Januari hadi Machi, 2022) Halmashauri iliendelea kukamilisha miradi ya fedha za bakaa na kuendelea kutekeleza Miradi kwa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kutoka vyanzo mbalimbali.

Aidha, ilifafanuliwa kuwa, miongoni mwa miradi iliyofadhiliwa na Wahisani ni pamoja na miradi iliyotekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko-19 ambapo Miradi hiyo imetekelezwa kwenye Sekta za Elimu na Afya. Jumla ya vyumba vya madarasa 16 vyenye thamani ya Sh. **320,000,000.00** vimejengwa katika Shule 9 za Sekondari, ujenzi wa Bweni lenye thamani ya Sh. **80,000,000.00** katika Shule ya Msingi Amani, ujenzi wa jengo la dharura (EMD) lenye thamani ya Sh. **300,000,000.00** katika Hospitali ya Mji Mafinga. Miradi mingine iliyotekelezwa yenye thamani ya jumla ya **Sh. 35,617,140.00** ni pamoja na ujenzi wa mifumo ya kunawia mikono, uvunaji wa maji ya mvua, uchimbaji wa visima virefu na uunganishwaji wa maji ya bomba katika Shule za Msingi 2 na Sekondari 1.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipongeza utekelezaji wa miradi husika kisha wakashauri kuwa ni vizuri fedha zikipelekwa ngazi za Kata kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ziadikwe na barua zitakazoonesha kuingizwa kwa fedha hizo kwenye akaunti husika.

MUHT: NA.20/HM/MAF/CMT/Q3/2021/2022- 08/04/2022: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo na kisha alifunga kikao mnamo saa 08:42 Mchana..

UMETHIBITISHWA LEO

JINA F. Kayunga

JINA Charles K. Tuyi

SAINI [Signature]

SAINI [Signature]

KATIBU

MWENYEKITI

TAREHE... 09/06/2022